

## Maswali ya Kila Mara kuhusu Vipimo vya COVID-19 Vilivyokwisha Muda

**Usitupe vipimo vyako vya COVID-19 vilivyokwisha muda. Hizi ni njia za kujua iwapo kipimo chako cha COVID-19 bado ni kizuri kutumia baada ya tarehe ya mwisho iliyoorodheshwa kwenye kisanduku.**

### **Je, naweza kutumia kipimo cha COVID-19 kilichokwisha muda?**

Ndiyo. Washington State Department of Health (DOH, Jimbo la Washington, Idara ya Afya) imetoa [uidhinishaji rasmi wa matumizi ya vipimo vilivyokwisha muda](#) (katika Kiingereza) almuradi vipimo hivyo vimepita udhibiti wa viwango, ambao tutaelezea hapa chini.

Isitoshe, vipimo vingine vya COVID-19 vilipokea ongezeko la muda wa kabla ya kuharibika kutoka kwa U.S. Food and Drug Administration (FDA, Utoaji wa Chakula na Dawa Marekani), ambalo linapatia vipimo hivyo tarehe mpya za kuisha muda tofauti na unachoona kwenye kisanduku. Unaweza kuangalia katika [Orodha za FDA za vipimo vilivyoongezewa muda](#) (katika Kiingereza na Kihispania) ili kuona vipimo ambavyo vimesasisishiwa tarehe ya kwisha muda. Hata kama kipimo kina tarehe mpya ya kuisha muda ambayo tayari imepita, kulingana na DOH, bado unaweza kutumia kipimo hicho iwapo kinaendana na udhibiti wa ubora.

Vipimo vya kwenda navyo nyumbani: Unaweza kutumia kipimo ambacho kimekwisha muda bora tu kinaendana na ukaguzi wa udhibiti wa ubora.

### **Nitajuaje kuwa kipimo cha COVID-19 kilichokwisha muda kitanipa matokeo sahihi?**

Kipimo chako cha COVID-19 kitakuja na ufafanuzi kuhusu hatua za kuchukua ili kuhakikisha kuwa kipimo kinafanya kazi vizuri, pia kinaitwa "udhibiti wa ubora." Huwa unaweza kupata mchakato wa udhibiti wa ubora katika sehemu ya matokeo ya kipimo kwenye karatasi ya maelekezo ya kipimo. Mchakato wa udhibiti wa ubora kwa vipimo vingi vya nyumbani ni kuhakikisha tu kuwa mstari kando ya "C" uliochapishwa kwenye kipimo unaonekana wakati ambapo sampuli imewekwa. Mchakato wa udhibiti wa ubora ukifeli, unafaa kutupa kipimo.

### **Kipimo huongezewa muda kiviipi?**

Watengenezaji wa vipimo vya COVID-19 wanahitajika kufanya utafiti unaoangalia muda ambao kipimo kinaweza kutumika. FDA hufuatilia data hii ili kuidhinisha tarehe za kwisha muda zilizoongezwa. Kuongezwa kwa tarehe za kwisha muda kwa vipimo vya COVID-19 ni kawaida kwani data nyingi huongezeka kuhusu muda ambao vipimo vinaweza kuchukua.

Tuna matumaini kwamba taarifa hii inakuhakikishia usalama unapotumia vipimo vilivyokwisha muda kutegemea tarehe ya kuisha kwa muda kwenye kisanduku. Sasa unajua jambo la kufanya ili kuona iwapo kipimo chako cha COVID-19 kiko sawa kutumiwa: fuata tu maelekezo ya kipimo ili kufanya udhibiti wa ubora. Kipimo kikipita udhibiti wa ubora, bado kipo salama na kizuri kutumiwa.

Asante kwa kila kitu huwa unafanya kulinda jamii zetu!

Ili kuomba hati hii katika muundo mwingine, piga simu kwa 1-800-525-0127. Kwa watu walio na ulemavu au matatizo ya kusikia, tafadhali piga simu kwa 711 ([Washington Relay](#)) au tuma barua pepe [civil.rights@doh.wa.gov](mailto:civil.rights@doh.wa.gov).